



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI
ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KAHAMA



Kumb. Na. KMC/F.20/23

22 Septemba, 2023

YAH: TANGAZO LA MIKOPO KWA WATUMISHI

Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama imepata mgao wa Fedha kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha kwa ajili ya Mkopo usio na Riba kwa Watumishi wa Umma ili waweze kununua Magari/Pikipiki, Samani na Matengenezo ya Magari/Pikipiki.

Kwa Tangazo hili Watumishi wote mnakaribishwa kutuma maombi kwa ajili ya Mkopo tajwa hapo juu chini ya masharti yafuatayo: -

- I. Mkopaji awe ni Mtumishi wa Umma wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama.
- II. Mkopo utazingatia kiwango kulingana na ngazi ya Mshahara na Mkopaji anatakiwa kubakiwa na 1/3 ya Mshahara wake baada ya Makato ambayo yatarejeshwa kwa kipindi kisichozidi Miezi 72.
- III. Mkopaji atalipa 'Service charge' (Gharama za kuandaa Mkopo) 3% na 'Protection Fund' (Ulinzi wa Mkopo) 1% kutoka kwenye Mkopo huo.
- IV. Mkopaji anatakiwa kutuma barua ya Maombi kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama.

Barua ya Maombi iambatishwe na Nakala ya Hati ya Mshahara ya Mwezi Agosti na Septemba, 2023.

Mikopo hii hainunui deni kutoka Benki au Taasisi nyingine za Fedha.

Maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama na Mwisho wa kutuma Maombi hayo ni tarehe **29 Septemba, 2023** saa Tisa Alasiri.

Limetolewa:

C.B. Mkusa
KAIMU MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MANISPAA
KAHAMA.

MUNICIPAL DIRECTOR
KAHAMA MUNICIPAL COUNCIL
P.O. Box 472
KAHAMA